




FAQ

Kiswahili



1. Sukuk ni nini?

Sukuk ni neno la kiarabu linalomaanisha hati fungani zinazozingatia misingi ya sharia za miamala ya kifedha ya kiislami.

Tofauti na hati fungani za kawaida(bonds) hati fungani hizi huwa na umiliki wa mali au manufaa kwa washirika walionunua hisa katika kuendesha miradi mbali mbali.

2. Ni zipi tofauti kati ya Ijarah Sukuk na Hati fungani za kawaida (Bondi)?

Kipengele	Ijarah Sukuk	Bondi
Umiliki	Inawakilisha umiliki wa mali	Inawakilisha deni
Mapato	Yanatokana na faida au kodi	Yanatokana na riba
Inazingatia Sharia	Ndio	Hapana
Uwepo wa mali halisi	Inahusisha mali halisi	Mara nyingi haina dhamana ya mali

3. Sukuk hutumika kwa ajili gani kwa ujumla?

Sukuk hutumika na Serikali au Makampuni ili kukusanya fedha kutoka kwa wawekezaji kwa kipindi fulani. Fedha hizi hutumika kufadhili miradi ya kibiashara au ya serikali kama vile ujenzi wa barabara, reli, mabwawa ya kuzalisha umeme, na mingineyo.

4. CRDB Al Barakah Sukuk ni nini?

CRDB Al Barakah Sukuk ni aina ya uwekezaji wa hati fungani iliyoundwa chini ya kanuni ya mkataba wa uwezeshaji wa Ijarah. Sukuk hii inawakilisha umiliki wa manufaa wa mali zilizopangishwa kupitia mdhamini (trustee).

5. Nini maana ya Ijarah Sukuk?

Hii ni hati fungani inayofuata miongozo ya uwekezaji inayokidhi vigezo vya sharia kwa mkataba wa Ijarah(ukodishaji) ambapo wawekezaji wa Sukuk humiliki sehemu ya pamoja ya mali kupitia mdhamini. Mtoaji wa Sukuk, akiwa kama mpangaji (lessee), hutumia mali hizo na hufanya malipo ya kodi(rentals) kwa vipindi maalum kwa wawekezaji wa Sukuk, ambayo ndiyo yanawakilisha faida ya uwekezaji wao.

6. Je CRDB Al Barakah Sukuk inafuata misingi ya Sharia?

Naam, CRDB Al Barakah Sukuk inafuata misingi ya uwekezaji wa sharia kwani imepitiwa na kuthibitishwa na waalam kutoka AlHuda Kituo cha Mabenki na Uchumi wa Kiislamu kilichoko Dubai, United Arab Emirates (UAE), ambao walikuwa Washauri wa Shariah na bodi ya usimamizi wa Sharia ya dirisha la huduma za kibenki zinazofuata misingi ya sharia CRDB Al Barakah.

7. Nani anatoa Sukuk ya Ijarah?

CRDB Bank PLC, kupitia dirisha ya CRDB Al Barakah Banking inatoa Ijarah Sukuk kwa wawekezaji wa kawaida na wa taasisi kama fursa ya uwekezaji inayozingatia misingi ya Shariah.

8. Mteja anapata Faida gani akiwekeza katika CRDB Al Barakah Sukuk?

Kwa kuwekeza katika CRDB Al Barakah Sukuk, mwekezaji/mteja atapata:



Usalama wa fedha katika kipindi chote cha uwekezaji.



Uhakika wa faida inayovutia katika kipindi kizima cha hati fungani.



Usalama wa fedha katika kipindi chote cha uwekezaji



Utulivu wa moyo kwa kuwekeza katika njia inayofuata misingi ya Sharia.



Mteja /Mwekezaji hata katwa kodi kwenye kuponi/Kuponi atakazowekewa.



Unaweza kuuza hatifungani yako ya Al Barakah katika soko la hisa la Dar es salaam kwa

kutegemea na uhitaji wa soko.

9. Kiwango cha faida cha CRDB Al Barakah Sukuk ni asilimia ngapi?



Kiwango cha faida cha 12% kwa mwaka, kitalipwa kila robo mwaka (mara 4 kwa mwaka) kwa uwekezaji utakaofanywa kwa shilingi za kitanzania



Kiwango cha faida cha 6% kwa mwaka, kitalipwa kila robo mwaka (mara 4 kwa mwaka) kwa uwekezaji utakaofanywa kwa dola za Marekani.

10. Je CRDB Al Barakah Sukuk ni kwa ajili ya wawekezaji waislam pekee?

Hapana, Al Barakah Sukuk ni kwa ajili ya kila mwekezaji, iwe ni mtu binafsi au shirika (Isipokua Biashara zisizozingatia misingi ya Sharia), bila ubaguzi wa dini wala rangi.

11. Ni kiasi gani mwekezaji/mteja anahitaji kuwekeza katika CRDB Al Barakah Sukuk?

Kiwango cha chini cha uwekezaji ni Shilingi 500,000 au Dola za Kimarekani 1,000 na kuendelea, hakuna kiwango cha mwisho cha juu cha uwekezaji.

12. Je CRDB Al Barakah Sukuk inakomaa baada ya muda gani?

Uwekezaji wa CRDB Al Barakah Sukuk unakoma baada ya miaka 5.

13. Nani anaweza kuwekeza kwenye CRDB Al Barakah Sukuk?



Watu binafsi (wenye umri wa miaka 18 au zaidi).



Watoto (kupitia mzazi au mlezi).



Vikundi.



Makampuni/taasisi (Isipokuwa biashara zisizozingatia misingi ya Sharia).



Raia wa Tanzania na wasiokuwa watanzania.



Wenza au wawekezaji wa Pamoja.



Watanzania waishio ughaibuni.



Wawekezaji wa nje.

14. Je, inawezekana kwa mtanzania mwenye account ya benki ya shilingi za kitanzania kununua dola za kimarekani kutoka kwa benki ili awekeze kwenye sukuk ya USD?

Hapana, mtanzania au muwekezaji mwenye account ya benki ya shilingi za kitanzania haruhusiwi kununua dola za kimarekani kutoka benki kwaajili ya kuwekeza kwenye sukuk. Muwekezaji mwenye account ya USD anaruhusiwa kuwekeza moja kwa moja kwenye Sukuk ya USD.

15. Mwekezaji atapokeaje kiasi cha awali cha uwekezaji katika CRDB Al Barakah Sukuk?

Malipo yote yatafanywa moja kwa moja kwenye akaunti ya mwekezaji iliyotolewa katika fomu ya maombi ya CRDB Al Barakah Sukuk.

16. Je, mwekezaji (mteja) anaweza kujaza akaunti isio na jina lake kama akaunti ya kupokelea gawio la faida?

Hapana, mwekezaji/mteja anapaswa kuweka akaunti yenye majina yake sahihi.

17. Je, mwekezaji/mteja anaweza kutumia Sukuk yake kama dhamana ya mkopo?

Ndio, mwekezaji/mteja anaweza kutumia CRDB AI Barakah Sukuk kama dhamana ya kuomba uwezeshaji unaofata misingi ya Shariah na kutumia gawio la faida kulipa kama rejesho au sehemu ya rejesho. Hii inategemea na vigezo na masharti kuzingatiwa.

18. Je, ninaweza kuuza AI Barakah Sukuk kabla ya muda wa ukomo?

Ndio, CRDB AI Barakah Sukuk inaweza kuuzwa kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa bei iliyoko sokoni.

19. Je, ratiba ya awamu ya kwanza ya utoaji wa AI Barakah Sukuk ipoje?

Tukio	Tarehe
Kufunguliwa kwa mauzo ya CRDB AI Barakah Sukuk	9 Agosti 2025
Kufungwa kwa ofa	12 Septemba 2025
Tarehe ya kuanza faida ya uwekezaji	8 Oktoba 2025
Tarehe ya kusajiliwa kwenye soko la hisa	17 Oktoba 2025
Ukomo wa uwekezaji wa CRDB AI Barakah Sukuk	8 Oktoba 2030
Tarehe za malipo ya faida	8 Januari, 8 Aprili, 8 Julai na 8 Oktoba

20. Mwekezaji/mteja anajiungaje na AI Barakah Sukuk?

Ili kuwekeza katika CRDB AI Barakah Sukuk, muwekezaji anaweza kujaza maombi;

1. Kupitia programu ya benki kupitia simu (SimBanking app)
2. Kupitia kujaza fomu ya maombi ya CRDB AI Barakah Sukuk iliyotolewa na tawi la CRDB, form kupitia tovuti ya CRDB au wakala wa hisa. Taarifa muhimu zinazopaswa kutolewa kwenye fomu:



Taarifa za Mwekezaji na anuani halisi



Taarifa za akaunti ya benki itakayopokea gawio la faida na kiasi cha cha uwekezaji wakati wa ukomo.



Akaunti ya CDS (kama hauna akaunti ya CDS utafunguliwa)



Kitambulisho halali - Kitambulisho cha Taifa, Pasipoti, Leseni ya Udereva, Kitambulisho cha mpiga kura, Kitambulisho cha Zanzibar Mkaazi



Kuweka kiasi cha uwekezaji cha TZS 500,000, USD 1,000 au zaidi kwenye akaunti ya CRDB AI Barakah iliyotajwa kwenye fomu ya maombi

21. Akaunti ya CDS ni nini?

Akaunti ya CDS inawakilisha mfumo wa kumbukumbu ya elektroniki ambao unaweka kumbukumbu za umiliki wa hati fungani zilizoshikiliwa na watu binafsi au taasisi na kurahisisha uhamisho wao. Mfumo huu unasimamiwa Dar-es-salaam stock exchange (DSE).

Mwekezaji anatakiwa kuwa na akaunti ya CDS ili kuwekeza kwenye CRDB AI Barakah sukuk.

22. Mwekezaji/mteja anapataje Akaunti ya CDS?

Iwapo mwekezaji/mteja hana namba ya akaunti ya CDS, itafunguliwa kwa kutumia taarifa zilizojazwa na mwekezaji/mteja kwenye fomu ya maombi ya CRDB AI Barakah Sukuk.

23. Je, mwekezaji/mteja anahitaji kuwa na akaunti ya benki na dirisha la huduma za kibenki zinazofuata misingi ya sharia za CRDB AI Barakah ili kuwekeza?

Ingawa wawekezaji wanaweza kutumia akaunti za benki nyingine kupokea gawio la faida, tunashauri mwekezaji/mteja kufungua akaunti na CRDB ili aweze kupata huduma za kibenki zinazofuata misingi ya sharia za kiislamu (AI Barakah Banking) ambayo itarahisisha kupokea gawio lake la faida.

24. Je, Kiwango cha faida kinaweza kubadilika?

Hapana, Kiwango cha faida (12% kwa mwaka) kwenye uwekezaji wa shilingi za kitanzania na (6% kwa mwaka) kwa wawekezaji wa dola za kimarekani hakitobadilika katika kipindi chote cha uwekezaji.

25. Mteja/mwekezaji anawezaje kukokotoa Kiwango cha faida atakayolipwa?

Kikokotoo kinapatikana kwenye tovuti ya CRDB. <https://crdbbank.co.tz/en>

Mfano; Al Barakah Sukuk ya TZS Milioni 100, itakayolipwa kwa miaka 5 kwa kiwango cha faida cha 12% kwa mwaka.

Mfano ukiwekeza	TZS 100,000,000
Faida ya mwaka	12% (TZS)
Kodi ya Zuiro	0%
Faida ya kila robo mwaka	3,000,000
Faida ya kila nusu mwaka	6,000,000
Faida ya kila mwaka	12,000,000
Faida kuu (Miaka 5)	60,000,000
Jumla (Uwekezaji + Faida)	160,000,000

26. Je, CRDB Al Barakah Sukuk inapatikana kwa sarafu za kigeni?

Ndio, CRDB Al Barakah Sukuk inapatikana kwa Dola za Kimarekani.

27. Je, Mwekezaji wa CRDB Al Barakah Sukuk anaweza kusitisha uwekezaji kabla ya tarehe ya ukomavu?

Hapana, uwekezaji ni kwa kipindi cha miaka 5. lakini, mwekezaji anaweza kuuza sehemu au kiasi chote kwenye soko la hisa la Dar es Salaam.

28. Iwapo mmiliki wa CRDB Al Brakah Sukuk amefariki nini kitatokea?

Umiliki wa CRDB Al Barakah Sukuk utahamishiwa kwa mrithi wa mali za marehemu aliyeidhinishwa kisheria.

29. Je, mwekezaji/mteja atapata cheti cha umiliki wa CRDB Al Barakah Sukuk?

Ndio, mwekezaji atapewa cheti cha umiliki wa Sukuk au risiti ya kidijitali kupitia SimBanking, pamoja na namba ya uthibitisho itakayoweza kutumika kufuatilia maelezo ya uwekezaji.

30. Je, Mteja/ Mwekezaji anaweza kuwa na Sukuk zaidi ya moja?

Mteja anaweza kuwekeza kwenye sukuk mara moja. Iwapo mwekezaji anataka kuongeza uwekezaji katika sukuk hii, anaweza kununua kwenye soko la hisa la Dar es Salaam kupitia mawakala waliothibitishwa.

Kwa maelezo au maswali ya ziada tafadhali wasiliana na sisi kupitia;

Barua Pepe: info@crdbbank.co.tz
Namba ya simu: +255(22)2197700 | +255(0)714197700 | +255(0)755197700 | 0800008000